MTANDAO WA MASHIRIKA YANAYOTETEA HAKI ZA ARDHI KWA WAZALISHAJI WADOGO NA WAFUGAJI WA ASILI TANZANIA
TANZANIA LAND ALLIANCE (TALA)

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSIANA NA HALI YA HAKI ZA ARDHI NCHINI

Dar es Salaam, 18 Novemba, 2011

Utangulizi

Sisi mashirika ya kiraia yanayotetea Haki za ardhi kwa Wazalishaji wadogo nchini (Wafugaji, Wakulima, Wachimbaji wadogo, Warina Asali na Waokota Matunda pamoja na Wavuvi), kwa muda mrefu tumekuwa tukifuatilia kwa ukaribu masuala ya utekelezaji wa Sera, Sheria na mikakati mbalimbali ya serikali katika utawala wa ardhi nchini. Ni dhahiri kwamba katika kipindi hiki cha miaka 50 ya uhuru wa nchi yetu, yapo mambo ambayo yamefanywa na serikali kwa ufanisi mkubwa katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya ardhi. Baadhi ya masuala hayo ni pamoja na; kuwepo kwa mfumo rasmi unaoratibu upatikanaji, umiliki na udhibiti wa ardhi kwa njia ya sera ya ardhi ya 1995, sheria za ardhi za 1999, sheria ya utatuzi wa migogoro ya 2002 na sheria nyinginezo zinazosadia utekelezaji wa vipengele muhimu katika sera ya ardhi na sheria hizo za msingi. Hata hivyo, licha ya kuwepo kwa sheria na miongozo hiyo yote, mashirika yetu yamekuwa yakishuhudia ukiukwaji mkubwa wa haki za ardhi na haki za binadamu kwa watu na jamii za wazalishaji wadogo wadogo kwa kiwango kikubwa sana. Baadhi ya maeneo ambayo kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria, kanuni na taratibu na usimamizi na umiliki wa ardhi na hivyo kusababisha athari kubwa kwa jamii husika pale inapotokea migogoro ni kama yafuatayo:

Kwanza, wimbi kubwa la **uhawilishaji** wa ardhi za vijiji kuwa ardhi ya jumla ikiwemo ardhi ambayo wanavijiji huitumia kwa uzalishaji, na kisha kuimilikisha kwa wawekezaji wakubwa wa ndani na nje ya nchi. Tafiti mbalimbali zilizofanywa na mashirika yetu zimeonyesha kuwa zoezi hili limekuwa likiambatana na vitendo vya ukiukwaji mkubwa wa haki za ardhi na haki za binadamu kwa wamiliki wa msingi wa ardhi inayohawilishwa. Tatizo la msingi katika eneo hili ni kwamba, uamuzi wa kuhawilisha ardhi

umekuwa ukifanywa kwa **mashinikizo** kutoka vyombo vya juu badala ya kuhusisha na **kuwashirikisha** kikamilifu wanavijiji wenyewe. Aidha, pale wanavijiji wanaposhiriki katika uamuzi, taratibu za kisheria hukiukwa kutokana na **kukosa uelewa** hasa katika kuendesha mikutano ya vijiji, kujadiliana na kufanya mapatano na wawekezaji na kuingia mikataba inayolinda maslahi yao kikamilifu. Mifano hai ni mikataba kati ya kijiji cha Idete wilayani Mufindi na Mwekezaji wa mradi wa hewa ya ukaa kutoka Norway uliohusisha hekta zaidi ya 11,000 wa mwaka 2008, ule wa kijiji cha Talawanda wilaya ya Bagamoyo na wawekezaji wa kuchimba mawe ya cement uliohusisha hekta 150 na kisha hekta 500 mnamo mwaka 2006 na 2007.

Pili, suala la **uwekezaji** kwenye ardhi za vijiji limekuwa chanzo cha uporaji wa ardhi ya wanavijiji bila kujali kuwa ardhi hiyo inatumika kwa ajili ya kujikimu na kuendesha maisha yao na kusababisha migogoro mikubwa na yenye athari lukuki kwa wananchi. Utafiti mdogo uliofanywa kupitia taarifa za vyombo mbalimbali vya habari umebaini kuwa, takribani migogoro mitano (5) huripotiwa kila siku ikihusisha wananchi na wawekezaji wa aina mbalimbali kwenye sekta za **utalii**, **madini**, **misitu** na hata **uwindaji**. Ukizingatia ukweli kuwa migogoro mingi inatokea katika maeneo ambayo hakuna vyombo vya habari na haitolewi taarifa, ni dhahiri kwamba kiwango cha migogoro ya ardhi kimeongezeka sana kutokana na wimbi hili la uwekezaji. Uwekezaji kwenye sekta ya madini tu peke yake, licha ya kusababisha uporaji wa ardhi kwa wenyeji umesababisha pia umasikini, migogoro baina ya wananchi na dhidi ya wawekezaji kuongezeka na kusababisha uvunjifu wa mara kwa mara wa haki Binadamu, yakiwemo mauaji ya watu wasio na hatia na uharibifu wa Mali.

Baadhi ya vyanzo vya msingi vya migogoro kati ya wawekezaji na wananchi ni pamoja na:

- wawekezaji wengi kutoa ahadi za uongo kwa wananchi ili kuwawezesha kupata ardhi lakini wakashindwa kuzitekeleza. Mfano wa ahadi ni pamoja na fursa za ajira, kuboreshewa miundombinu,

kufanya tathmini ya athari za kimazingira, kutoa huduma za jamii kama vile elimu, afya na maji n.k. hivi karibuni tulishuhudia wananchi wa vijiji 11 vinavyozungukwa na mashamba ya mwekezaji wa sun biofuel na uongozi wa wilaya ya Kisarawe wakimlalamikia mwekezaji huyo kwa kushindwa kutimiza ahadi ya kuajiri wafanyakazi 5,000 na badala yake kuajiri 750 ambao hata hivyo wameachishwa kazi kutokana na mwekezaji huyo kuuza mradi wake kwa mwekezaji mwingine.

- Sababu nyingine ni wawekezaji wanaobadili matumizi ya ardhi tofauti na yale waliyoombea ardhi hiyo na wapo pia wanaodiriki kujiongezea maeneo zaidi ya waliyokubaliana na wananchi.

- Aidha kuna wawekezaji ambao hupewa ardhi na kisha kuvuna rasilimali zilizomo bila kuwekeza kitu chochote na kuamua kutelekeza ardhi hiyo. Mfano hai ni mwekezaji wa zao la jatropha aitwaye bioshape ambaye alipewa ardhi inayofikia hekta 36,000 lakini aliishia kuvuna mbao kisha kuacha ardhi hiyo ikiwa pori hadi leo huko wilaya ya Kilwa.

- Wawekezaji kutofuata taratibu za kisheria na kuamua kuwatumia baadhi ya watu wenye ushawishi katika jamii na hasa wafanyabiashara na wanasiasa kupata ardhi. Inapokuwa vigumu kupata ardhi kwa mtindo huu, vyombo vya dola vimekuwa vikitumika kuwaondosha wananchi katika maeneo yao ili wapishe wawekezaji kwa nguvu. Kinachotokea bonde la Kiru na Loliondo mara kwa mara ni sehemu ya aina hii ya uwekezaji.

Tatu, suala la **usimamzi na utawala** wa ardhi kwa ujumla wake limekuwa na matatizo makubwa. Baadhi yake ni pamoja na:

- Serikali kushindwa kupima maeneo, kupanga matumizi na kusimamia uendelezaji wa ardhi katika vijiji, ardhi ya jumla na hifadhi. Matokeo yake, kumekuwa na matatizo kadha wa kadha kuhusiana na uvamizi

wa maeneo ya wazi, watu kujichukulia hatua mkononi ikiwemo kukodisha vikundi binafsi vya ulinzi kudhibiti ardhi yao n.k

- Kushindwa kutekeleza wajibu wake wa msingi wa kuelimisha watumiaji wa ardhi na kusimamia utekelezaji wa sheria jambo ambalo limesababisha ukiukwaji mkubwa wa haki za ardhi kwa wazalishaji wadogo na wanyonge waishio vijijini.

Nne, mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi licha ya kuwa ni dhaifu kwa namna mbalimbali lakini pia umekuwa ukiingiliwa na vyombo vya utawala wakiwemo wanasiana na watendaji. Mwaka jana, Mkuu wa mkoa mmoja alithubutu kuingilia shauri lililokuwa linaendelea kwenye baraza la ardhi na nyumba la wilaya, akaamuru shauri likomee hapo na kufunga ofisi za baraza hilo. Hali kadhalika, mabaraza ya ardhi ya vijiji na kata licha ya kuwa ni machache na hayana uwezo kwa vile hayajajengewa uwezo, bado yanaingiliwa na watendaji katika ngazi hizo na hata wanasiasa wakiwemo madiwani wa kata husika. Hii ni kuingilia mkondo wa utoaji wa haki na vyombo visivyohusika na kuzidi kuwadidimiza wanyonge.

Kutokana na hayo yote na mengine mengi ambayo hayawezi kuainishwa katika tamko hili fupi, mashirika yetu yanatoa tamko hili kwa lengo la kuikumbusha serikali wajibu wake wa msingi wa kuhakikisha kila mtanzanzia anakuwa na uhakika wa kupata na kumiliki ardhi ikiwa ni pamoja na kunufainika na ardhi yake kwa namna mbalimbali. TALA tunatamka na kuitaka serikali kufanya mambo yafuatayo ili kurejesha hali ya amani, milki za ardhi na haki za msingi miongoni mwa jamii za wazalishaji wadogo ambazo zimeporwa na kuathiriwa kwa namna mbalimbali:

1. Serikali isitishe maramoja uwekezaji wa aina yoyote kwenye ardhi za vijiji na katika maeneo yote ambayo hayajapimwa hadi pale upimaji wa vijiji na maeneo hayo utakapofanyika ili kutambua na kulinda kwanza haki za wenyeji kabla ardhi haijagawiwa kwa wawekezaji.

2. Ardhi yote ya Tanzania ipimwe kwa mkakati maalumu (kama ule wa sensa ya watu) ili kubaini na kutenga maeneo kulingana na shughuli husika na kuruhusu uhifadhi wa maeneo yenye rasilimali zenye umuhimu wa kipekee kwa taifa. Hii inatokana na ukweli kuwa baadhi ya wawekezaji wamemilikishwa maeneo yenye kiasi kikubwa cha baoanuai na hata yanayofaa kuwa hifadhi maalumu za mazingira.

3. Sheria ya Ardhi itambue na kutamka bayana kuwa gesi, Madini na Mafuta ni sehemu ya ardhi na uwekwe utaratibu mahsusi wa kuzivuna rasilimali hizo kwa namna ambayo wananchi wa maeneo husika wananufaika. Kwa mfumo wa sasa, wananchi wanaoishi katika maeneo yenye rasilimali hizo hulazimika kuhama au kuhamishwa kwa nguvu ili kupisha uwekezaji mkubwa.

4. Kumekuwa na uwekezaji unaoendelea katika madini ya urani sehemu mbalimbali nchini. Hata hivyo bado hakuna uratatibu wowote wa kisheria wala mfumo wa usimamizi wa shughuli hii nyeti na yenye athari kubwa kwa jamii. Tunaitaka serikali isimamishe maramoja mipango yoyote ya uchimbaji wa Madini ya Urani hadi hapo uchambuzi yakinifu kuhusu athari zake utakapofanyika.

5. Tunatambua kuwa uwekezaji wa aina mbalimbali ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa letu. Endapo ni lazima baadhi ya wananchi kuondoka katika maeneo yao kupisha uwekezaji, basi fidia kamili, ya haki na ya wakati ilipwe sambamba na kuwepo kwa mfumo unaowafanya wananchi hao kuwa wabia wa uwekezaji badala ya kuwafukuza kwa mtutu wa bunduki.

6. Suala la wawekezaji kuchangia maendeleo kwa jamii limefanywa kuwa la hiyari. Athari zake zimekuwa kubwa kwavile, mali ya thamani kubwa inachukuliwa huku michango ya wawekezaji kwenye

maendeleo ikiwa midogo sana. Tunaitaka serikali itunge sheria ili kuwafanya wawekezaji wawe na wajibu kisheria katika kuchangia maendeleo ya vijiji ambako uwekezaji unafanyika na kusimamia ahadi zinazotolewa wakati wa kutwaa ardhi za vijiji.

7. Upimaji na utoaji wa hati na vyeti vya kimila umekuwa ukisuasua. Kwa mujibu wa hotuba ya bajeti ya wizara ya ardhi ya mwaka huu wa 2011(uk 11) wizara imetoa jumla ya hatimiliki za kimila 157,968 ambacho ni kiasi kidogo sana kwa wakazi wan chi hii wanaofikia milioni 45 na vijiji zaidi ya elfu 11. Tunaitaka serikali kuharakisha uandaaji na utoaji wa hati na vyeti hivi ili kupunguza migogoro na kusaidia kuwapa uhakika wa milki wananchi husika. Aidha mchakato wa kupatikana kwa Hati Milki za Kimila uwekewe muda maalum kwa Kamishna wa Ardhi kwani zimekuwa zikichukua muda mrefu sana kukamilika na kutolewa kwa wahusika.

8. Vijiji viachiwe mamlaka kuingia makubaliano na wawekezaji wao wenyewe bila kuingiliwa na mamlaka zinginge kama vile wanasiasa na Halmashauri za Wilaya/Serikali kuu ambao wamekuwa hawawezeshi maslahi ya wanavijiji kulindwa. Endapo unatakiwa utaalamu basi wanavijiji wahusishwe kuwapata wataalamu wanaowataka bila kushururishwa.

9. Mamlaka ya Rais katika ardhi iondolewe ili vyombo vyenye uwakilishi mpana wa wananchi ndivyo viwe na mamlaka zaidi. Hii inatokana na ukweli kuwa mamlaka ya milki ya hatma aliyo nayo Rais imekuwa ikitumiwa vibaya na watendaji anaowakasimu au watendaji kutumia jina la Rais kuhalalisha maamuzi yao.

10. Suala la operesheni za kuwaondoa wafugaji katika maeneo yao bila mipango madhubuti lisitishwe maramoja kwani limekuwa likisababisha usumbufu mkubwa kwa jamii hizo na hasa wanawake na watoto pamoja na kuwarudisha nyuma kiuchumi jamii husika.

Mifano hai ya operesheni za Loliondo, Meatu, Ihefu na Kilosa ni ushahidi tosha kwa hoja hii.

11. Kumekuwa na mgongano kati ya Sera na Sheria za ardhi na sheria mbalimbali na maoni yametoloewa mara kwa mara migongano hii iondolewe. Hata hivyo serikali imekuwa ikisuasua kufanya marekebisho hayo. Ni rai yetu kuwa sasa ni wakati muafaka kwa serikali kuondoa migongano hii kwa kubadili sheria zote zenye mgongano na zinazodidimiza haki za wananchi

12. Serikali ihakikishe kuwa mfumo wa utendaji kazi wa Kituo cha Uwekezaji (TIC) unabadilishwa mara moja pamoja na kutumia taarifa sahihi kuhusu ardhi iliyopo nchini inayofaa kwa uwekezaji badala ya kutumia taarifa zilizopitwa na wakati au za kukisia.

Imetolewa na

_____

Tanzania Land Alliance- TALA

HAKIARDHI

LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

MVIWATA

LHRC

WLAC

Ujamaa Community Resource Team